

**MUONGOZO WA USAHIHISHAJI
ELIMU YA DINI YA KIISLAMU.
KIDATO CHA NNE 2024**

1. Mtahiniwa anatakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kati ya majibu aliyopewa katika kipengele cha kwanza hadi cha kumi.

1@Alama 1= Alama 10

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.
C	D	D	E	C	B	D	B	C	A

2. Mtahiniwa anatakiwa kuoanisha nguzo za imani katika Orodha A na aya zinazokamilisha katika Orodha B kisha andika herufi ya jibu katika sehemu ya kuandika majibu aliyopewa.

1@Alama 1= Alama 10

Orodha A	i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.
Orodha B	C	F	E	D	B	A

3. Mtahiniwa anatakiwa kuandika Matunda ya Kusimama Uislamu katika Jamii kama ifuatavyo.

Hoja 6 @ hoja 1 alama 1.5 jumla Alama 9.

- Humukombo mwanaadamu kutokana na kila aina ya utumwa na umiliki wa kibinaadamu. Humfanya mwanaadamu kuwa muadilifu na mtenda wema katika maisha yake yak kila siku.
- Humfanya mwanaadamu awe mpole na mwenye huruma kwa wanaadamu wenziwe na viumbe wengine.
- Humfanya mwanaadamu (muumini) awe mvumilivu, jasiri, mwenye subira katika kusimamia haki na usawa katika jamii.
- Humfanya mwanaadamu awe mwenye kukinai na kutosheka kwa kile alichoruzukiwa na Muumba wake.
- Kusimama Uislamu katika jamii ndio hupatikana maisha ya amani na furaha ya kweli katika jamii.
- Humuwezesha mwanaadamu kuwa na mtazamo mpana na sahihi juu lengo la maisha yake.
- Huwezesha mwanaadamu kuondosha na kuzuia kila aina yak uovu na uchafu katika maisha yak jamii.

4. Mtahiniwa anatakiwa kuandika umuhimu wa ndoa katika jamii.

Hoja 6 @ hoja 1 alama 1.5 jumla Alama 9.

- Kuhifadhi jamii na zinaa
Ndoa hukinga wanandoa na jamii kwa ujumla na zinaa kwa kuhifadhi tupu zao na kukidhi matamanio baina yao. Rejea Qur'an (5:5), (4:24)
- Kuendeleza kizazi cha mwanaadamu kwa utaratibu mzuri
Lengo la ndoa pia ni kuhifadhi, kutunza na kuendeleza kizazi cha mwanaadamu bila kuzaliana kiholela. Rejea Qur'an (4:1), (42:11)

- iii. Kujenga mapenzi, huruma na ushirikiano katika familia
Ndoa huleta utulivu katika moyo kati ya wanandoa na kupatikana huruma, mapenzi na ushirikiano baina yao Rejea Qur'an (30:21), (2:187)
 - iv. Kukuza uhusiano na udugu katika jamii
Uhusiano na udugu kati ya wanafamilia walioana huimarika na kuongezeka zaidi kuwa ukoo, kabilia, taifa, n.k Rejea Qur'an (25:54), (49:13)
 - v. Kukilea kizazi katika maadili
Ndoa inakusudiwa kuwa kiungo cha kulea na kuelimisha kizazi katika tabia na maadili mema anayoyeridhia Allah (s.w).
 - vi. Kumuendeleza mwanaadamu kiuchumi
Ndoa huchochea wanandoa na wanajamii kwa ujumla kujijenga kiuchumi ili kukidhi mahitaji muhimu ya kimaisha na kibinaadamu. Rejea Qur'an (6:151)
5. Mtahiniwa anatakiwa kuandika haki za mwanamke katika uislamu kwa kuandika hoja zifuatazo.

Hoja 6 @ hoja 1 alama 1.5 jumla Alama 9.

- i. Haki ya mwanamke kupata elimu
Kujielimisha ni amri kwa wanaume na wanawake, sio wanaume pekee. Rejea Qur'an (96:1-5)
 - ii. Haki ya mwanamke katika sitara
Ni haki kwa mwanamke kupata kulingana na asili ya maumbile yake. Rejea Qur'an (33:59), (24:31)
 - iii. Haki ya mwanamke katika uchumi
Kama ilivyo kwa mwanamume ana haki ya kuchuma na kumiliki uchumi, mwanamke pia ana haki hiyo. Rejea Qur'an (4:32), (4:4)
 - iv. Haki ya mwanamke katika jamii (ndoaa, mirathi na talaka)
Mwanamke ana haki ya kuolewa na mwanamume anayemridhia kwa kuzingatia sheria za Kiislamu kwa hiari. Rejea Qur'an (4:7)
 - v. Haki ya mwanamke katika sharia
Mwanamume na mwanamke wana haki sawa mbele ya sheria katika kuhukumiwa, kuadhibiwa, kudai haki, n.k. bila ya ubaguzi wowote. Rejea Qur'an (5:38), (24:2). Mwanamke kama mwanamume, ana haki ya kutoa ushahidi mahakamani pale inapobidi. Rejea Qur'an (2:282)
 - vi. Haki ya mwanamke kushiriki katika uongozi na siasa
Jukumu la kuendesha maisha ya jamii liko kwa mwanamume na mwanamke katika kuamrisha mema na kukataza mabaya.
Suala la uongozi wa kifamilia na kijamii ni la wote, mwanamume na mwanamke isipokuwa mwanamke haruhusiwi kuwa kiongozi wa nchi. Rejea Qur'an (9:71), (58:1-4)
6. Mtahiniwa anatakiwa kuonyesha utofauti kati ya Mfumo wa Uchumi wa Kiislamu na ule wa Kitwaghuti.

Hoja 3 @ hoja 1 alama 3 jumla Alama 9.

Uchumi wa Kiislamu	Uchumi wa Kitwaghuti
1. Dhana ya mafanikio Huzingatia hatima yake ambayo ni kupata radhi za Allah (s.w) pekee.	Huzingatia kiasi cha mali alichokichuma na kukimiliki mtu.
2. Dhana ya umilikaji mali	Mmiliki ni mwanaadamu anayehusika na

Mmiliki hakika wa pekee wa mali na rasilimali zote ni Allah (s.w).	kuchuma, kuzalisha na kusambaza.
3. Dhana ya bidhaa Ni kitu kilicho safi, kizuri, twahara, halali, n.k.	Ni kitu chochote kinachowenza kutumiwa na mtu au watu.
4. Dhana ya matumizi Haifai kufuja au kutumia mali au rasilimali kwa njia za haramu.	Mtu anauhuru wa kufuja na kutumia mali au rasilimali apendavyo.
5. Mizani ya wakati katika kutumia Ni kujiuliza, nini matokeo ya mali au rasilimali hiyo baada ya muda fulani?	Ni kujiuliza, kiasi gani cha mali au rasilimali mtu awe nacho baada ya muda fulani?

7. Mtahiniwa anatakiwa kuandika madhara ya riba katika jamii kwa kuandika hoja zifuatazo *Hoja 5 @ hoja 1 alama 1.8 jumla Alama 9.*

- i. Riba inachafua nafsi ya tajiri, kwa kuwa bahili, mchoyo asiyetayari kuwasaidia maskini, wanyonge na wenyewe shida mpaka bila malipo yeyote ya ziada.
- ii. Riba huchafua mali ya tajiri kutokana na njia haramu za kuchuma na kumiliki bila kuzingatia mipaka.
- iii. Riba inakandamiza wanyonge, maskini na wenyewe dhiki na matatizo, wenyewe kuhitajia misaada ili waweze kuishi.
- iv. Riba inaharibu uchumi na maendeleo ya jamii kwa kudhulumu kundi la maskini na kufaidisha kundi la matajiri.
- v. Riba inahamisha uchumi, mali na rasilimali kutoka kwa maskini na wanyonge kwenda kwa matajiri.

8. Mtahiniwa anatakiwa kuandika hoja zinazothibitisha kuwa Qur-an ni Neno la Allah (s.w) kwa kutumia Qur-an yenyewe kwa kuandika hoja zifuatazo:

Hoja 6 @ hoja 1 alama 1.5 jumla Alama 9.

- i. Kutojua kusoma na kuandika kwa Mtume Muhammad (s.a.w)
Mtume (s.a.w) kutojua kusoma na kuandika ni ushahidi tosha kuwa asingeweza kutunga Kitabu mfano wa Qur'an. Rejea Qur'an (7:158), (29:48)
- ii. Qur'an yenyewe inajieleza kuwa ni Kitabu cha Allah (s.w) kama ifuatavyo; "Uteremsho wa Kitabu hiki umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima" (45:2). Pia rejea Qur'an (4:166), (32:2-3), (35:31), (25:1), n.k
- iii. Hali aliyokuwa nayo Mtume (s.a.w) wakati akipokea wahyi
Mtume (s.a.w) alikuwa akiogopa kuwa atasahau anayoteremshiwa, akawa na pupa kuyakariri, hii ni ushahidi kuwa hayakuwa maneno yake. Rejea Qur'an (75:16-18), (87:6-7)
- iv. Qur'an kushuka kidogo kidogo kwa kipindi cha miaka 23 kimatukio.
Kama Qur'an aliitunga Mtume (s.a.w) angeliitunga yote kwa pamoja tena kwa haraka ili kuitumia kuongoza jamii. Rejea
- v. Mtume (s.a.w) kukosolewa ndani ya Qur'an.
Kama Mtume Muhammad (s.a.w) angelikuwa ndiye mtunzi wa Qur'an asingelikosolewa mara nyingi katika Kitabu alichokitunga mwenyewe.
Rejea Qur'an (33:1-3), (66:1), (80:1-12), n.k
- vi. Kutokea kweli matukio yalitabiriwa katika Qur'an

Mifano ya matukio ni; Waislamu kuwashinda Warumi na Maquishi na kuwa katika hali ya furaha na amani, utabiri wa kuangamia Abu Lahab. Rejea Qur'an (30:2-3), (111:1-5), (93:4-5), (94:5-6), (48:1), n.k

- vii. Mpangilio na muundo wa aya na sura za Qur'an wakati wa kushuka kwake na kuandikwa katika msahafu.
Aya na sura za Qur'an zimepangiliwa ki-idadi na kimuundo kwa namna ya ajabu ambayo hakuna mwanaadamu yeoyote anayeweza kufanya hivyo. Mfano: neno mbingu saba limetajwa mara saba, neno "Yaum" (siku) limetajwa mara 365, neno "shahri" (mwezi) limetajwa mara 12, n.k. Rejea Qur'an (3:59), (2:87), (2:33-37), (20:115-121), n.k
- viii. Wanaadamu kushindwa kutunga na kuandika Kitabu mfano wa Qur'an Qur'an imetoa changamoto kwa kuwataka wanaadamu kutunga kitabu au sura moja au aya moja tu mfano wa Qur'an hakuna aliyeweza. Rejea Qur'an (17:88), (11:13), (2:23), (10:38), n.k
- ix. Maudhui ya Qur'an na mvuto wa ujumbe wake
Qur'an inaathiri na kugonga nyoyo za watu hata ambao si waislamu, mfano Umar Ibn Khattab na mshairi Labib ibn Rabiah kabla ya kusilimu. Rejea Qur'an (20:1-7), (4:82),
- x. Ahadi ya Kuhifadhiwa na kulindwa Qur'an na kubakia katika asili yake
Ni Qur'an pekee ambayo mwanaadamu hawezি kukiharibu kwa namna yeoyote ile ya kuongeza au kupungaza chochote. Rejea Qur'an (15:9)
9. Mtahiniwa anatakiwa kuandika hoja za makafiri juu ya uwepo wa Allah (s.w) na udhaifu wa madai yao kwa kuandika yafuatayo.

Utangulizi alama 2

Hoja 6@ hoja 1 alama 2 = 12

Hitimisho alama 1

Jumla alama 15.

kafiri wa zamani na wa zama hizi wakiwemo Charles Darwin, Friedrich Engles, n.k wanadai kuwa imani ya uwepo wa Mungu Muumba dhana tu haina dalili yeoyote. Miiongoni mwa hoja (madai) zao wanazotoa ni hizi zifuatazo;

- i. **Mwenyezi Mungu hayupo kwa sababu haonekani na wala hadirikiki kwenye milango ya fahamu.** Rejea Qur'an (17:90-92).

Milango ya fahamu kama vile macho katika kumuona, pua katika kumnusa, masikio katika kumsikia, ngozi katika kumhisi au kumgusa pia, n.k

Udhaifu wa hoja hii,

Milango ya fahamu ina udhaifu mwingi sana na kikomo pia, kama vile macho au pua huweza kuona au kunusa vitu viliyo karibu tu na visivyokuwa na kizuizi, kuna vitu vingi vinavyotuzunguka lakini hatuvioni kama upепо, sauti, n.k.

- ii. **Mwenyezi Mungu amefanywa kuwepo na wanadamu kutohara fikra na mawazo duni na uduni wa maendeleo ya sayansi na teknolojia.**

Hii ni baada ya mwanaadamu kushindwa kutatua matatizo katika mazingira yake na hivyo kuibukia kujundia muingu.

Udhaifu wa hoja hii,

Historia inaonyesha kuwa hakuna zama mwanaadamu aliishi bila ya ujuzi wa kukabiliana na mazingira yake, Mwanaadamu wa kwanza kuumbwa alipewa ujuzi (elimu) ya kukabilana na mazingira yake na hatimaye kushushiwa muongozo kamili wa maisha kutoka kwa Muumba wake. Rejea Qur'an (2:31,38).

iii. **Hapana Mungu Muumba bali vitu vyote vimetokana na mabadiliko ya kimaada.**

Wanadai kuwa maumbile na viumbe vyote vinatokana na mabadiliko kidogo kidogo ya kimaada (evolution) baada ya muda mrefu kupita kutoka hali moja kwenda nyingine. Mfano binaadamu kutoka pweza, mjusi, sokwe na hatimaye mtu kamili.

Udhaifu wa hoja hii,

Nadharia hii haina ushahidi wowote wa kisayansi, kiuchunguzi na utafti bali ni dhana tu aliyoibuni Darwin ili kupotosha uhalisia na ukweli juu ya chanzo cha maumbile. Hadi leo hii hakuna mwanasayansi ye yote anayeweza kuthibitisha nadharia hii.

iv. **Kama Mungu Muumba yupo, ni ipi nasaba (ukoo) yake au ametokana na nini?**

Makafiri wa zamani na sasa wanasingizia kutoamini kuwepo Mungu kwa kuwa hawajui nasaba, ukoo au asili yake anatokana na nani au na nini.

Udhaifu wa hoja hii,

Kwa kutumia mantiki, Muumba wa vitu vyote ndiye chanzo na asili ya vitu vyote. Hivyo ni lazima asiwe na nasaba, mwanzo au mwisho pia. Na asitokane na vitu au maumbile yale. Rejea Qur'an (112:1-4).

v. **Vitu havikuumbwa bali vimetokea kwa bahati nasibu (by chance) na vitatoweka kwa bahati nasibu pia muda wake ukifika.**

Makafiri wa zamani na sasa wanadai kuwa asili ya maumbile yote yametokana na bahati nasibu (by chance), hivyo vitatoweka kama vilivyoibuka.

Udhaifu wa dai hili,

Hakuna uwezekano wa kuwepo maumbile bila ya Muumbaji na msimamizi mwenye ujuzi na uwezo wa hali ya juu na mtegemewa wa kila kitu, kwani kila kitu kinachoonekana kimeumbwa na kimewekwa kwa lengo maalum.

vi. Hakuna mungu bali mwanadamu huamini kibubusa na kufuata mkumbo tu bila dalili au kutumia akili.

Udhaifu wa dai hili.

Maana ya neno "IMANI" ni kuwa na yakini moyoni kuwepo kwa jambo usiloniona ila una dalili za kutosha za kuthibitisha kuwepo kwa jambo hilo. Hivo maana tu ya IMANI inakanusha dai hilo.

10. Mtahiniwa anatakiwa kuandika ufufuo kutokana na historia katika Qur-ani ambapo kuna matukio ya kihistoria yanayothibisha kuwepo uhai baada ya kufa.

Utangulizi alama 2

Hoja 6@ hoja 1 alama 2 = 12

Hitimisho alama 1

11. *Jumla alama 15.*

- i. Mtu (msafiri) na punda wake waliokufa walifufuka baada ya miaka mia (100).Rejea Qur'an (2:259)
 - ii. Kufufuka ndege wanne (4) wa Nabii Ibrarrahim (a.s) kama mujiza wa kuonesha uwezekano wa kufufuliwa viumbi.Rejea Qur'an (2:260)
 - iii. Kuamka vijana wa pangoni baada ya kulala kipindi cha muda wa miaka 309 ili kuwa ushahidi wa kufufuka viumbi baada ya kufa.Rejea Qur'an (18:25)
 - iv. Kufufuka kwa watu wa Nabii Musa (a.s) waliokufa walipotaka kumuona Allah (s.w) kwa dhahiri (jahara).Rejea Qur'an (2:55-56)
 - v. Kufufuka kwa mtu (Myahudi) aliyeuliwa kwa dhuluma zama za Nabii Musa (a.s) ili amtaje aliyemuua baada ya kupigwa na sehemu ya nyama ya ng'ombe.Rejea Qur'an (2:72-73)
 - vi. Nabii Isa (a.s) kufufua wafu (watu waliokufa) kwa idhini ya Allah (s.w) kama sehemu ya muujiza wake.Rejea Qur'an (3:49), (5:111)
12. Mtahiniwa anatakiwa kuandika hoja zinazolezea kwanini lengo la hija halifikiwi kwa kuandika hoja zifuatazo:
- Pamoja na mkusanyiko wa mamillioni wa mahujaj katika Mji wa Makka kila mwaka lakini matunda ya Hijra hayafikiwi. Zifuatazo ni baadhi ya sababu;
- Utangulizi alama 2*
- Hoja 6@ hoja 1 alama 2 =12*
- Hitimisho alama 1*
- Jumla alama 15.*

- i. Kuhiji kwa chumo la haramu.
Waislamu wengu hufunga safari ya kwenda hija kwa fedha za pato la haramu ambazo ni kikwazo cha kupata matunda ya hija zao.
- ii. Kutochunga niuko, nguzo na sharti za Hijah.
Pamoja na kufunga safari ya Hijah au Umrah, mahujaj wengi hawachungi niuko, nguzo na masharti ya Hijah au Umrah ipasavyo.Rejea Qur'an (2:197).
- iii. Kutokuwa na elimu na ujuzi sahihi juu ya ibada ya Hijah.
Mahujaji wengi hufunga safari ya kwenda Hijra au Umrah ili hali hawana ujuzi wowote wa ibada watakazozitekeleza ila kufuata mkumbo tu.
- iv. Kutojulikana kwa lengo halisi la Hijah au Umrah.
Waislamu wengu hufunga safari ya Hijah au Umrah kwa lengo la kupata thawabu na kufutiwa madhambi tu na sio kuwa askari wa kupigania dini. Rejea Qur'an (51:56).
- v. Kufunga safari ya Hijah kwa Malengo mengine.
Waislamu wengu hufunga safari kwa ajili ya biashara, utalii au kutafuta umaarufu wa kuijiita majina ya Al-Hajj ambayo ni nje na lengo la Hijah.